
Hapo zamani za kale, wanyama wote walikuwa wanaishi katika nchi ya Kitasha.Nchi hiyo ilikuwa nzuri na neema tele. Ilikuwa na misitu minene na milima mirefu mizuri.

Mvua zilikuwa nyingi, na mito ilitiririka kutoka milimani wakati wote. Chakula kilikuwa kingi. Twiga hakuwa na sababu ya kunyoosha shingo yake ndefu kutafuta majani kwenye miti mirefu. Swala nao hawakupata shida ya kupata majani laini. Majani yalipatikana kwa wingi kando kando ya vijito.

Siku hizo mwenyekiti wa wanyama alikuwa Tembo. Mwenyekiti Tembo aliitisha mkutano wa wanyama wote.

Lengo la mkutano huo ilikuwa kutafuta ufumbuzi wa tatizo la maji. Wanyama wote waliitika wito wa mkutano, wakaja kwa wingi. Sungura peke yake hakufika kwenye mkutano. Mwenyekiti Tembo alifungua mkutano na kuwashukuru wajumbe wote kwa kufika. Kisha aliwaeleza wajumbe kusudi la mkutano huo.





Alisema, “Ndugu wajumbe mliohudhuria mkutano huu, natumaini kila mmoja wetu anafahamu tatizo la ukosefu wa maji linalotukabili katika nchi yetu. Tatizo hili limedumu kwa muda mrefu. Hakuna dalili kuwa litamalizika siku za karibuni kwa sababu hakuna dalili yoyote ya mvua. Hivyo basi ninawaomba kila mmoja wetu afikiri ni kwa jinsi gani pamoja tutaweza kulitatua tatizo hili.”

Kadiri siku zilivyopita, ndivyo wanyama walivyoharibu mazingira yao. Walikata miti ovyo na kulima kwenye vyanzo vya maji. Pamoja na hayo, walichoma moto misitu.

Kutokana na uharibifu huu wa mazingira, mvua hazikunyesha. Mito yote na mabwawa yalianza kukauka. Ukame huo uliendelea kwa muda mrefu. Mazao yote yalikauka, hivyo kukawa na shida kubwa ya maji na chakula.

Fisi alikuwa wa kwanza kuchangia mawazo. Alinyoosha mkono na mara aliporuhusiwa akasema, “Mimi napendekeza kuwa tushirikiane kuchimba kisima kikubwa kitakachotosheleza mahitaji yetu ya maji.”

Pendekezo la Fisi lilikubalika na wanyama wote. Wanyama wote kwa kauli moja, wakakubaliana kazi ianze mara moja, kwa kuwa tunaona wote hali tuliyonayo inazidi kuwa mbaya. Walipanga kuanza kazi hiyo siku inayofuata asubuhi na mapema. Mwenyekiti aliwataka wajumbe wote wawahi ili waanze kazi mapema kabla jua halijawa kali.



Siku iliyofuata wanyama wote isipokuwa Sungura, walichukua vifaa kama majembe, sululu, sepeto na vifaa vingine vingi kwa ajili ya kuchimba kisima.


Kutokana na tabia ya uvivu, ujeuri na kutopenda kushirikiana na wenzake, Sungura hakufika kuchimba kisima.

Kazi ya kuchimba kisima ilianza asubuhi na mapema na iliendelea vizuri. Ilipofika saa kumi jioni, maji mengi yalipatikana. Kwa furaha wanyama walishangilia na kuimba, “Maji, maji, maji.”

Sungura aliposikia kelele za wanyama wakishangilia alijua kuwa maji yamepatikana. Baada ya kazi kukamilika, mwenyekiti aliangalia huku na kule lakini hakumwona Sungura. Aliwauliza wanyama wengine kama wamemwona Sungura.

Nyani akanyoosha mkono akasema, “Mimi sijamwona lakini najua jinsi sungura alivyo mjeuri mjanja na asivyopenda kazi na ushirikiano na wenzake, huenda ndiyo maana hakuweza kuja.”

Mbwa mwitu ambaye alikuwa mkuu wa ulinzi aliwapangia wanyama wote zamu za kulinda kisima. Fisi alikuwa wa kwanza kuwa na zamu ya kulinda.



Siku iliyofuata, Sungura alijihimu mapema asubuhi na kwenda kisimani kuchota maji. Alipofika kisimani alimkuta Fisi amekaa. Sungura hakutaka kumwonyesha kuwa alitaka kuchota maji.

Baada ya kusalimiana, Fisi akamwuliza kwa mshangao, “Hee,unakwenda wapi asubuhi yote hii?” Sungura hakutaka kumwambia kuwa amekuja kuchota maji. Sungura kwa kuwa ni mjanja alianza kumpa Fisi maneno ya uongo.

Alimdanganya kuwa, anaelekea kwenye karamu. Alimwambia Fisi, “Unajua ndugu yangu, leo kuna karamu kubwa kwa Simba. Ametafuta kitoweo kingi, akaamua kutualika wote tukashiriki. Sherehe yenyewe inaanza sasa hivi asubuhi. Twende zetu tuwahi kabla hawajafika wanyama wengi.”

Fisi alikubali kuondoka na Sungura kwenda kwenye sherehe nyumbani kwa Simba. Baada ya kwenda kitambo kidogo, ghafla Fisi alimuona Sungura anasimama.

Fisi alimuuliza mbona umesimama? Sungura alimwambia Fisi kuwa anataka kwenda kujisaidia hivyo kama atapenda amsubiri arudi ndipo waendelee na safari.

Kumbe Sungura alimdanganya Fisi. Alirudi kisimani akateka maji, na kuoga kisha akayachafua sana. Fisi alipoona Sungura harudi, aliamua kurudi nyumbani. Hakwenda kwa Simba wala hakurudi tena kulinda kisima.

Huku nyuma asubuhi wanyama wengine walipofika kisimani kunywa maji walikuta maji yamechafuka sana. Fisi ambaye alikuwa analinda kisima hawakumuona pia.

Walimtafuta na walipompata, walimwuliza ilikuwaje hadi maji yote yamechafuliwa kiasi kile. Wanyama wote waliendelea kumuuliza kwa nini hakuwepo kwenye lindo kama walivyokubaliana.

Fisi hakuthubutu kuwaeleza alichoambiwa na Sungura, hivyo alikaa kimya tu. Waliendelea kumuuliza sana ndipo alisema ukweli. Alisema kuwa Sungura alimwambia wamealikwa kwenye sherehe ya simba, lakini walipokuwa njiani Sungura alimtoroka.

Wanyama wote walikasirika sana, walipanga kumtafuta Sungura na kumwadhibu. Fisi naye walimpa adhabu ya kuishi kwa kula makombo na mifupa kwa kutofanya kazi yake vizuri.




Zamu iliyofuata ilikuwa ya Swala. Aliwahakikishia wanyama wenzake kuwa atatumia mbinu zote mpaka amkamate Sungura. Sungura kama kawaida yake alitaka kwenda kuchota maji kisimani. Alikwenda kwa kunyemelea ili amwone ni nani yuko zamu.

Alimwona Swala akilinda. Alirudi nyumbani kuchukua upinde na mshale. Akajificha kichakani karibu na kisima. Mara akatoa mshale na kumlenga Swala. Mshale ulianguka karibu sana na Swala.

Loo! Swala alishtuka sana kuona mshale unaanguka karibu yake. Akaona kuwa amekoswakoswa kuuawa na mwindaji. Bila kusita wala kusubiri, Swala alitimua mbio na kurudi nyumbani na kuacha kisima bila ulinzi.

Sungura alipoona Swala amekimbia alikwenda kuchota maji kisha akaoga na kuyachafua sana. Wanyama wengine walipofika kisimani kunywa maji walishangaa sana kwani walikuta yamechafuliwa tena. Walikasirika kwelikweli, wakamwita Swala aje kueleza ilikuwaje mpaka maji yakachafuliwa tena.

Swala akiwa bado anatetemeka aliwaambia wanyama wenzake kuwa alipokuwa analinda alikoswakoswa kuuawa hivyo akakimbia na kuliacha lindo. Wanyama walipouona ule mshale, walimsikitikia na kumhurumia kwa kunusurika kuuawa.



Hata hivyo, wanyama hawakukata tamaa. Waliapa kuendelea kulida mpaka wamkamate huyo mhalifu. Kobe alisema yeye atalinda tena akaahidi kuwa atamkamata.

Hivyo, siku iliyofuata Kobe alikwenda kulinda. Sungura bila kuchelewa siku hiyo alifika kisimani, na alipoangalia huku na kule hakuona mlinzi.

Hakuweza kumwona Kobe kwa sababu alikuwa ameficha kichwa na miguu yake akaonekana kama jiwe pembeni mwa kisima.Sungura alijaribu kuita kirafiki na kwa sauti kubwa. “Halo, halo rafiki, nina habari njema ya kukueleza.”

Alifanya hivyo kwa kuwa alifikiri kuwa pengine mlinzi alikuwa amejificha kichakani. Aliongeza sauti yake tena lakini hakumwona mlinzi.

Sungura alifurahi sana kuona kuwa hapakuwa na ulinzi siku hiyo. Hivyo aliamua kuchota maji kisha kuoga ndani ya kisima kwa uhuru kabisa. Alipomaliza alianza kuyachafua maji.

Ghafla Kobe alimrukia na kumkamata mkia huku akipiga kelele,“Mwiziii... Mwiziii... Mwizi jamani. Nimemkamata nisaidieni.”

Waliendelea kuangushana mieleka na hatimaye wanyama wengine walianza kuja kumsaidia Kobe kumkamata mhalifu.

Wanyama wote walifurahi sana kumpata mhalifu wao. Walijadiliana jinsi ya kumuadhibu. Tembo akasema achinjwe na ipikwe supu apewe mzee Simba ambaye ni mgonjwa.

Sungura aliposikia adhabu hiyo, alianza kulia na kuomba msamaha. Lakini hakuna aliyemhurumia. Nyati alileta kisu kikali, akapewa Mbwa mwitu ili amchinje.

Mbwa Mwitu alinoa kisu chake. Sungura alipoona kuwa sasa anakufa, aliamua kujitoa kwa nguvu kutoka mikononi mwa Mbwa Mwitu.

Mbwa Mwitu akakirusha kisu kwa nguvu sana kikampata Sungura mkiani. Sungura akakatika mkia na kukimbilia kichakani.

Wanyama wote walimkimbiza lakini hawakuweza kumkamata. Kobe alibaki na kipande cha mkia. Ndiyo maana Sungura ana mkia mfupi mpaka leo na pia anaishi kwa wasiwasi wakati wote kwani anaogopa kukamatwa.

